## Miradi ya maendeleo katika Mkoa

**Mpango Wa Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now- BRN)***

Sekta ya Kilimo katika Mkoa wa Rukwa inatekeleza mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)* katika Halmashauri za Wilaya ya Kalambo na Sumbawanga kwa lengo la kuongeza uhakika wa chakula na kufanya Kilimo kuwa cha kibiashara. Katika Mkoa wetu Mpango huu unashughulika na mazao ya mahindi na Mpunga. Mkoa una Jumla ya maghala 110 yenye uwezo wa kuhifadhi mazao tani 92,328. Miongoni mwa maghala hayo, maghala 32 yaliyopo katika maeneo yanayolima mahindi kwa wingi yameanishwa kwa ajili ya kukarabatiwa chini ya mpango wa BRN ili kuanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani na kuwaunganisha wakulima na masoko ya mahindi.

***Jedwali Na. 13: Idadi ya maghala yaliyopo katika Halmashauri za Mkoa wa Rukwa na Uwezo wa Kuhifadhi mazao.***

| **Halmashauri** | **Idadi ya maghala** | **Uwezo wa kuhifadhi mazao (tani)** |
|---|---|---|
| Sumbawanga *(M)* | 55 | 64,728 |
| Sumbawanga *(W)* | 16 | 10,000 |
| Kalambo | 20 | 12,850 |
| Nkasi | 19 | 4,750 |
| **Jumla** | 110 | 92,328 |

*Chanzo: Taarifa za Halmashauri*

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2015/2016 jumla ya maghala 9 yalipagwa kukarabatiwa katika Halmashauri ya wilaya ya Kalambo. Mpaka sasa ukarabati huo upo katika hatua mbalimbali za ukarabati.

Kupitia BRN Skimu ya umwagiliaji ya Sakalilo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga itakamilishiwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, Wakulima watapatiwa mafunzo ya kuzalisha mpunga kibiashara na kupatiwa mbinu za utafutaji wa masoko ya zao la mpunga ndani na nje ya nchi. Ujenzi wa mifereji yenye urefu wa mita 2200 ya kupeleka maji mashambani upo katika hatua za mwisho.

**Programu ya MIVARF**

Program ya kuendeleza Miundombinu ya Masoko, Uongezaji thamani mazao na Huduma za Kifedha Vijijini *(MIVARF)* ilianza kutekelezwa Mkoani kwetu mwaka 2012/2013 katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Program hii inalenga kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la mpunga ambapo imesaidia ukarabati wa ghala la mazao lenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,500 katika kijiji cha Kaoze kwa gharama ya shs. 55,671,700/-. Aidha, Program inalipia gharama za kuwajengea uwezo jamii ya wakulima wa mpunga kupitia vikundi 9 katika Kata tano (5) zilizopo bonde la Ziwa Rukwa za Muze, Mtowisa, Milepa, Ilemba na Kaoze.

Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuunda na kusajili vikundi 4, ufunguaji wa akaunti benki, elimu ya ujasiliamali, utafutaji masoko ya mazao na kuwaunganisha vikundi na Taasisi za fedha, elimu ya Stakabadhi ghalani na mafunzo ya Kilimo biashara. Katika msimu wa Kilimo wa 2014/2015 walihifadhi jumla ya gunia za mpunga 720 (Kg.57,600) ambazo walifanya mauzo yake mwezi Novemba 2015 kwa kupeleka kwenye soko la Mbeya ambapo walipata jumla ya shilingi 57,600,000.00.

Halmashauri za Kalambo na Nkasi zimeingizwa kwenye Programu mwaka 2015/2016 na 2016/2017 kujengewa miundombinu ya

kuhifadhi samaki wabichi. Hii ni kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la samaki mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Hatua iliyopo sasa katika utekelezaji wa mradi huo, amepatikana Mshauri Mwelekezi wa uhandisi ili kuandaa michoro *(design)* kwa kuyaboresha masoko hayo. Masoko yaliishajengwa lakini hayakukamilika ili yatumike kikamilifu, moja ya Miundombinu itakayoongezwa ni kujenga vyumba vya barafu *(Cold rooms)* na kuweka vifaa vyake ili kuweza kuhifadhi samaki wabichi.

**Programu ya Uendelezaji wa zao la ngano**

Mkoa kwa kushirikiana na Taasisi ya Kilimo Uyole tunaendesha programu ya Kilimo cha ngano katika Halmashauri zote za Mkoa wa Rukwa. Katika programu hiyo tunatoa mafunzo ya Kilimo bora cha ngano kwa wakulima waliojiunga katika vikudi, tunaendesha mashamba darasa katika vijiji na kuweka mashamba ya mfano katika baadhi ya vijiji vya mradi. Tayari Wadau wa zao la ngano wameunda Jukwaa lao linalojulikana kwa jina la JUNGARU *(Jukwaa la Wadau wa Ngano Mkoa wa Rukwa).* Kazi kubwa ya Jukwaa hili ni kuhakikisha kuwa zao la ngano linalimwa kitalaamu na kuwaongezea wadau kipato. Katika msimu wa 2015/16 Jukwaa kwa kushirikiana na Halmashauri waliweza kuwaunganisha wakulima na kampuni ya TFC na kukopeshwa kiasi cha tani 33 za mbolea zenye thamani ya shilingi 42,900,000.00 kwa wakulima wa ngano ambao ni wanachama wa JUNGARU.

Hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2017 Jumla ya shilingi 42,204,000.00 zimesharejeshwa TFC sawa na asilimia 98.4. Bado kiasi cha shilingi 696,000.00 sawa na asilimia 1.6.

Katika msimu wa 2016/2017 wakulima hao waliopo kwenye vikundi wanaendelea na Kilimo cha ngano kwa kutumia mitaji yao katika kununua pembejeo za Kilimo.

## MFUKO WA TAIFA WA JAMII (TASAF III)

Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa Mikoa inayotekeleza TASAF awamu ya tatu – Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini zilizo katika Mazingira Hatarishi. Mpango huu unanusuru Kaya Maskini kutokana na athari za Umaskini na kuziwezesha kupata mahitaji ya msingi, kulinda rasilimali zao na kuwekeza kwa maendeleo yao.

### Hali ya Utekelezaji

TASAF awamu ya tatu katika Mkoa wa Rukwa ilipanga kuzifikia takribani kaya **23,221** katika Halmashauri zote za Mkoa kwa vijiji na mitaa **285**

***Mchanganuo wa Vijiji na idadi ya kaya zinazonufaika na mpango wa TASAF***

| Na | Halmashauri | Idadi ya Vijiji/mitaa | Idadi ya Kaya nufaika |
|---|---|---|---|
| 1 | Nkasi | 54 | 5,533 |
| 2 | Sumbawanga | 71 | 6,190 |
| 3 | Kalambo | 66 | 4,678 |
| 4 | Manispaa ya Sumbawanga | 94 | 6,820 |
| **JUMLA** | | **285** | **23,221** |

Katika kipindi cha malipo kwa Kaya Masikini cha kuanzia Julai, 2015 hadi Agosti, 2016 kiasi cha **Shilingi 6,640,904,500.57** zimekwishapokelewa kwa ajili ya Uhaulishaji wa fedha kwa Kaya Masikini, Usimamizi na Ufuatiliaji wa shughuli za Mpango kutoka

TASAF Makao Makuu (TMU) na kuweza kuzilipa Kaya Masikini **23,221** katika vijiji/mitaa **279. Vijiji 6** kati ya **285** vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ni Vijiji vya Mlinganisho ambavyo vinategemewa kuanza kupokea fedha baada ya **miezi 18** tangu zoezi la uhaulishaji wa fedha kuanza katika Halmashauri hiyo.